TANGAZO LA SERIKALI NA. 598 la tarehe 25/8/2023

SHERIA YA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA,
(SURA YA 306)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 103(2))*

# KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA ZA KUSIMAMIA HUDUMA ZA UTANGAZAJI ZA JAMII ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

### SEHEMU YA PILI
### UENDESHAJI WA KITUO CHA HUDUMA ZA UTANGAZAJI WA JAMII

4. Misingi ya kituo cha huduma za utangazaji wa jamii.
5. Umiliki wa kituo cha huduma ya utangazaji wa jamii.
6. Majukumu ya kituo cha huduma za utangazaji za kijamii.
7. Vyanzo vya mapato.

### SEHEMU YA TATU
### MAUDHUI YA KITUO CHA UTANGAZAJI CHA JAMII

8. Maudhui ya vipindi.
9. Maudhui ya matangazo.
10. Maudhui yanayokatazwa.
11. Vipindi vya dini.

### SEHEMU YA NNE VIGEZO VYA KIUFUNDI

12. Kituo cha redio.
13. Kituo cha televisheni.

TANGAZO LA SERIKALI NA. 598 (*Linaendelea*)

SHERIA YA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA,
(SURA YA 306)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 103(2))*

KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA ZA KUSIMAMIA HUDUMA ZA UTANGAZAJI ZA JAMII ZA MWAKA 2023

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta za Kusimamia Huduma za Utangazaji wa Kijamii za mwaka 2023.

Matumizi

**2.-**(1) Kanuni hizi zitatumika katika huduma za utangazaji za jamii Tanzania Bara.

(2) Malengo ya Kanuni hizi yatakuwa kuweka miongozo kwa-

(a) waombaji wa leseni wanaotaka kuanzisha huduma za utangazaji za jamii; na

(b) wamiliki wa leseni kuhusu namna watakavyosimamia na kuendesha huduma za utangazaji za jamii.

Tafsiri

**3.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"huduma za utangazaji za jamii" maana yake ni huduma za maudhui ya utangazaji yanayotolewa bila kipato kwenye jamii husika.

"jamii" maana yake ni kundi la watu wanaoishi katika eneo moja la kijiografia na yenye sifa za kipekee au maslahi ya pamoja;

Sura ya 172

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania;

"matangazo ya jamii" maana yake ni matangazo madogo yasiyokuwa na sura ya kibiashara yenye lengo la kuchangia gharama za uendeshaji wa kituo cha utangazaji wa jamii;

TANGAZO LA SERIKALI NA. 598 (*Linaendelea*)

"maudhui" maana yake ni taarifa kwa namna ya hotuba au sauti, data, maandishi au picha mnato au jongefu, isipokuwa pale ambapo taarifa hiyo inarushwa kwa ajili ya mawasiliano binafsi;

"mtoa huduma ya maudhui ya kijamii" maana yake ni chombo kilichoidhinishwa kutoa huduma za utangazaji kwa njia ya redio au televisheni katika jamii fulani, chombo kinamilikiwa na jamii hiyo na kutoa huduma kwa msingi usio wa kibiashara; na

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta.

## SEHEMU YA PILI
## UENDESHAJI WA KITUO CHA HUDUMA ZA UTANGAZAJI WA JAMII

Misingi ya kituo cha huduma za utangazaji wa jamii

**4.** Kituo cha huduma za utangazaji wa jamii kitakuwa na misingi ifuatayo-

(a) vipindi vitakuwa mahsusi kwa ajili ya wanajamii wa jamii husika kwa madhumuni yasiyokuwa ya kibiashara;

(b) kitakusudia kutoa huduma katika eneo husika au jamii yenye maslahi, mienendo na utamaduni unaofanana;

(c) kitatoa fursa kwa wanajamii wa jamii husika kuwasiliana na kushiriki katika uandaaji wa vipindi vya kituo cha utangazaji;

(d) kitahudumia jamii iliyokusudiwa;

(e) kitawajibika kwa jamii husika;

(f) kitamilikiwa, kusimamiwa na kuendeshwa na jamii husika;

(g) hakitaendeshwa kwa madhumuni ya kibiashara;

(h) hakitaanzishwa au kuendeshwa kwa misingi ya kidini au kisiasa;

(i) muundo na uendeshaji wake utazingatia muundo wa uongozi wa jamii husika; na

(j) vipindi vitalenga mahitaji ya elimu, maendeleo, jamii na utamaduni wa jamii husika.

Umiliki wa kituo cha huduma ya utangazaji wa jamii

**5.-**(1) Umiliki na uendeshaji wa kituo cha utangazaji wa jamii utakuwa kupitia-

(a) taasisi za elimu ya juu na taasisi nyingine za elimu;

(b) mamlaka za serikali za mtaa;

(c) chama cha kijamii, bodi ya udhamini au mifuko ya kijamii;

TANGAZO LA SERIKALI NA. 598 (*Linaendelea*)

(d) mashirika yasiyo ya kiserikali; na

(e) jamii nyingine yeyote kama Mamlaka itakavyoona inafaa.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ya 5(1)(a) hadi (e) kituo cha huduma ya utangazaji wa jamii hakitaruhusiwa kumilikiwa na kuendeshwa na wafuatao-

(a) vyama vya kisiasa;

(b) watu binafsi;

(c) taasisi za kidini;

(d) mashirika ya kibiashara; na

(e) makundi mengine yeyote ambayo hayajihusishi na maslahi ya jamii.

(3) Waombaji wa leseni ya huduma za utangazaji wa jamii watawasilisha azimio lililosainiwa na wawakilishi wa jamii husika likiahidi kutii Kanuni hizi.

Majukumu ya kituo cha huduma za utangazaji za kijamii

**6.** Kituo cha huduma za utangazaji za kijamii kitakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kutoa huduma ya utangazaji ya jamii katika eneo husika la kijiografia;

(b) kukuza vipaji na utengenezaji wa maudhui ya ndani;

(c) kuhamasisha jamii kushiriki kwenye shughuli za maendeleo;

(d) kujengeana uwezo kupitia kubadilishana taarifa ndani ya jamii husika;

(e) kuhamasisha utawala bora katika jamii husika;

(f) kuchochea ukuaji wa maendeleo ya kijamii kwa kutengeneza vipindi vyenye maudhui yanayokidhi mahitaji ya elimu, afya, uchumi, biashara, maendeleo, mazingira, sayansi na utamaduni kwa kushirikisha jamii husika;

(g) kuhamasishana juu ya uelewa wa masuala mbalimbali ili kukabiliana na changamoto kwenye jamii husika;

(h) kusaidia kufikia muafaka na kuendeleza malengo ya pamoja kupitia midahalo na majadiliano ya masuala ya kijamii;

(i) kukuza utamaduni wa sanaa na ubunifu wa jamii husika; na

(j) kuhamasisha amani, umoja, ulinzi na usalama, mshikamano, utulivu na utaifa.

Vyanzo vya

**7.-**(1) Vyanzo vya mapato vya kituo cha huduma ya

mapato

utangazaji cha jamii yatakayotumika kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa kituo cha utangazajivitakuwa kama ifuatavyo-

(a) fedha zitokanazo na michango, misaada, matangazo ya kijamii, na vyanzo vinginevyo vya kihisani;

(b) fedha kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo walioidhinishwa na mamlaka husika; na

(c) udhamini wa Serikali au mashirika yasiyo ya kibiashara.

(2) Kituo cha huduma ya utangazaji cha jamii hakiruhusiwi kuwa na chanzo chamapato kinachotokana na biashara yoyote.

## SEHEMU YA TATU
## MAUDHUI YA KITUO CHA UTANGAZAJI CHA JAMII

Maudhui ya vipindi

**8.** Maudhui ya kituo cha utangazaji chaijamii yatazingatia yafuatayo:

(a) kuakisi mahitaji muhimu na malengo ya jamii katika kuhamasisha maendeleo, afya, elimu, mazingira, ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii, uchumi, sayansi, teknolojia na utamaduni;

(b) maudhui yanayotangazwa na kituo yanapaswa kuwa angalau asilimia themanini (80%) za vipindi vinavyoshirikisha jamii katika eneo kituo kilipoanzishwa;

(c) kutumia lugha ya taifa ya Kiswahili isipokuwa pale Mamlaka itakapotoa kibali maalum; na

(d) kutunza maudhui ya vipindi vinavyotangazwa kwa miezi mitatu kuanzia siku ya urushaji wa vipindi husika.

Maudhui ya matangazo

**9.** Matangazo na udhamini vitazingatia yafuatayo-

(a) matangazo ya kijamii yatahusu eneo husika na huduma za maendeleo;

(b) wadhamini wa vipindi hawatakiwi kuingilia uendeshaji wa kituo, maudhui na namna vipindi vinavyoendeshwa;

(c) kwa kuzingatia masharti ya kanuni hii, urushaji wa matangazo ya kijamii na udhamini hautazidi dakika tano kwa saa.

Maudhui yanayokatazwa

**10.** Kituo cha huduma ya utangazaji cha jamii hakiruhusiwi kutangaza vipindi vyenye maudhui yafuatayo:

(a) yasiyo na staha na yenye kukosa uadilifu kwa mujibu wa mila na desturi za jamii husika;

(b) yanayochochea ubaguzi au kushambulia imani za kidini,

TANGAZO LA SERIKALI NA. 598 (*Linaendelea*)

itikadi za kisiasa, jamii, kabila, ishara au kuleta madhara yanayoweza kupelekea uvunjifu wa amani katika jamii;

(c) yanayohamasisha vitendo vya ngono, ponografia, udhalilishaji, kashfa, uongo, udanganyifu au upotoshaji;

(d) yanayotweza shughuli na mienendo ya serikali, bunge na mahakama;

(e) yanayochochea ponografia ya watoto.

Vipindi vya dini

**11.** Kituo cha huduma ya utangazaji cha jamii kitahakikisha kwamba kinakua makini kuhusu vipindi vya dini na kuepuka yafuatayo:

(a) masuala nyeti yanayoweza kuibua hisia hasi za kidini; na

(b) kufanya kosa juu ya maoni ya dini na imani kwa walio katika dini au dhehebu fulani.

## SEHEMU YA NNE
## VIGEZO VYA KIUFUNDI

Kituo cha redio

**12.** Kituo cha redio ya jamii-

(a) kitaruhusiwa kujenga miundombinu ya utangazaji kwa kuzingatia viwango vya kiufundi vilivyoidhinishwa na Mamlaka; na

(b) kitarusha matangazo kwa kuzingatia Kanuni za Ubora wa Huduma na kanuni nyinginezo kama zitakavyokuwa zimeidhinishwa na Mamlaka.

Kituo cha televisheni

**13.** Kituo cha televisheni cha jamii-

(a) kitaruhusiwa kujenga studio ya kuandaa na kurusha matangazo kwa kuzingatia viwango vya kiufundi vilivyoidhinishwa na Mamlaka;

(b) kitarusha maudhui yake kupitia kwa mbeba maudhui (MUX) aliye katika eneo la kijiografia la jamii husika; na

(c) kitaingia makubaliano ya huduma na mbeba maudhui kwa ajili ya usambazaji wa matangazo.

Dar es Salaam,
................, 2023

**JABIRI K. BAKARI**
*Mkurugenzi Mkuu*